

# **JINSI YA KUFANYA MAANDALIZI YA SIKU YA USHAIRI WA WATOTO DUNIANI (WoChiPoDA)**



**Shairi ni mchezo wa maneno ambao huleta kicheko baada ya siku ya furaha au siku ya huzuni.**

**~ Gloria D. Gonsalves**

- 1. Chagua kikundi cha watoto (chini ya miaka kumi na nne) na lengo lako k.m. watoto wa shule, watoto yatima, watoto walio hospitali, watoto wa mtaani, watoto kutoka jamii fulani, n.k.**
- 2. Amua idadi ya watoto unayoweza kumudu maandalizi.**
- 3. Chagua eneo la sherehe k.m. ukumbi wa matukio, nyumba binafsi, ufukweni, n.k.**
- 4. Ikiwa hauna ujuzi wa sanaa ya mashairi, mshirikishe mwanashairi au mwalimu wa mashairi.**
- 5. Mashairi yanaweza kuwa katika mtindo wowote, juu ya chochote na kwa lugha yoyote. Mtandao una maelezo mengi kuhusu utungaji na uandishi wa mashairi k.m. [mashairi ya kimapokeo](#) na [mashairi ya kimamboleo](#).**
- 6. Kuwa huru kuchagua mada ya sherehe k.m. mazingira, wanyama, mimea, n.k.**

- 7. Fikiria kutafuta udhamini wa kuchangia kiasi cha gharama au gharama zote k.m. kukodisha ukumbi, burudani, utengenezaji wa bango, n.k.**
- 8. Washirikishe vyombo vya habari ili kuipatia sauti maadhimisho ya sherehe hii. Waweza kulitangaza tukio la WoChiPoDa kupitia tangazo au makala gazetini.**
- 9. Tangaza tukio la sherehe hii kwa kutumia jina la mwandalizi wa adhimisho k.m. “Shaaban Mtanga anawaletoa /Shule ya Msingi Mabawa inawaletoa Siku ya Ushairi wa Watoto Duniani 2018”.**
- 10. Mwanzilishi wa siku hii, [Gloria D. Gonsalves](#), atambuliwe pia pale inapoonekana sahihi. Watoto hupendelea kumuita jina la “Auntie Glo” au “Shangazi Glo”.**

\*\*\*\*\*